TANGAZO LA SERIKALI NA. 22 la tarehe 20/1/2023

SHERIA YA FEDHA ZA UMMA,
(SURA YA 348)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 17(1))*

AMRI YA KUANZISHA MFUKO WA MAENDELEO YA KILIMO YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo ya Mwaka 2023.

Tafsiri

2. Katika Amri hii, isipokuwa kama muktadha utahitajivinginevyo-

Sura ya 348

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Fedha za Umma;

"Mfuko" maana yake ni Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo ulioanzishwa chini ya aya ya 3;

"Katibu Mkuu" maana yake ni Katibu Mkuu mwenye dhamana na masuala ya Kilimo ambaye pia atakuwa afisa masuuli wa Mfuko;

"kilimo" maana yake ni kilimo-mazao, miundombinu yake na shughuli nyingine zinazohusiana na maendeleo ya kilimo; na

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana na masuala ya kilimo.

Uanzishaji wa Mfuko

3. Unaanzishwa Mfuko maalum utakaojulikana kama Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo au kwa kifupi "MMAKI".

Madhumuni ya Mfuko

4. Madhumuni ya Mfuko yatakuwa ni kugharamia maeneo ya kimkakati yanayojitokeza kwa umuhimu ili kuchochea ukuaji na maendeleo ya kilimo.

Majukumu ya Mfuko

5. Majukumu ya Mfuko yatakuwa ni-

(a) kuwezesha uwekezaji katika miundombinu ya kilimo kama vile uzalishaji, maghala, usindikaji, usafirishaji na masoko kwenye mnyororo wa thamani inapotokea uhitaji;

(b) kuimarisha upatikanaji wa pembejeo za kilimo, zana za kilimo na ruzuku pale itakapohitajika;

(c) kufidia bei za mazao inapotokea hasara iliyosababishwa na majanga ya asili au mdororo wa uchumi;

(d) kuchochea uwekezaji kwenye uzalishaji wa mazao kwa kuzingatia viwango vya ubora wa soko la ndani, kikanda na kimataifa;

(e) kuwezesha utengaji na ulinzi wa maeneo ya ardhi ya kilimo kwa ajili ya maendeleo ya kilimo;

(f) kuwezesha uhaulishaji na uhamasishaji wa matumizi ya teknolojia za kilimo kwa wakulima na wadau wa kilimo; na

(g) kugharamia uendeshaji, usimamizi, ufuatiliaji na shughuli nyingine zinazohusiana na kazi za maendeleo ya kilimo.

Usimamizi wa Mfuko

6. Mfuko utasimamiwa na Katibu Mkuu ambaye ndiye atakuwa afisa masuuli wa Mfuko akisaidiwa na watumishi wa Wizara ya Kilimo watakaoteuliwa kutoka kada mbalimbali kama itakavyohitajika kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Mfuko.

Kamati ya Ushauri

7. Kutakuwa na Kamati ya Ushauri wa Mfuko ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Katibu Mkuu - Wizara ya Fedha na Mipango ambaye atakuwa ni Mwenyekiti;

(b) Katibu Mkuu - Wizara ya Kilimo ambaye atakuwa ni Katibu;

(c) Katibu Mkuu - Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;

(d) Katibu Mkuu - Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara;

(e) Mrajisi wa Vyama vya Ushirika;

(f) Mwenyekiti wa Umoja wa Mabenki Tanzania; na

(g) Katibu wa Baraza la Kilimo Tanzania.

Majukumu ya Kamati ya Ushauri

8. Majukumu ya Kamati ya Ushauri yatakuwa-

(a) kumshauri Katibu Mkuu kuhusu matumizi ya Fedha za Mfuko;

(b) kupitia taarifa ya uchambuzi wa maombi ya fedha za mfuko na kupendekeza kwa Katibu Mkuu;

(c) kuidhinisha mpango mkakati, mpango wa biashara wa Mfuko na bajeti ya mfuko kwa kila mwaka wa

fedha;
(d) kumshauri Katibu Mkuu kuhusu vyanzo vipya vya mapato ya Mfuko;
(e) kupitia taarifa za ufuatiliaji na tathmini ya matumizi ya fedha zilizotolewa;
(f) kuidhinisha taarifa za kila mwaka na taarifa za fedha zilizokaguliwa;
(g) kuidhinisha miongozo ya maombi ya fedha na vigezo vya utoaji wa fedha;
(h) kuweka utaratibu wa ukusanyaji na uchangiaji wa vyanzo vya mapato vya Mfuko;
(i) kuhakikisha fedha zote za vyanzo vya mapato ya Mfuko zinakusanywa na kuingizwa kwenye akaunti ya Mfuko;
(j) kutoa ushauri kwa Katibu Mkuu kuhusu suala lolote litakaloonekana muhimu kwa ajili ya maendeleo ya kilimo; na
(k) kuidhinisha miongozo ya usimamizi wa Mfuko.

Vyanzo vya fedha za za Mfuko

9. Vyanzo vya fedha za Mfuko vitakuwa ni pamoja na-
(a) fedha za Mfuko kama zitakavyoidhinishwa na Bunge;
(b) michango na misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo;
(c) asilimia hamsini ya tozo ya mauzo ya korosho ghafi nje ya nchi;
(d) tozo kwa mazao ya kilimo yanayosafirishwa kwenda nje ya nchi kwa mujibu wa viwango vilivyobainishwa kwenye Kanuni za Sheria ya Afya ya Mimea;
(e) michango ya mifuko ya udhamini ya kuendeleza mazao kwa kiwango kitakachoidhinishwa na Bodi husika au kupitia mjengeko wa bei kwa zao husika;
(f) riba itakayotokana na uwekezaji wa muda mfupi;
(g) vyanzo vya fedha vitakavyoainishwa katika sheria nyingine;
(h) asilimia 0.05 ya CIF kwa mazao ya kilimo yanayoingizwa nchini kwa mujibu wa viwango vilivyobainishwa kwenye Kanuni za Sheria ya Afya ya Mimea; na
(i) vyanzo vingine vya mapato kama itakavyoamriwa

na Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha kwa kushauriana na Waziri.

Matumizi ya fedha za Mfuko

10.-(1) Katibu Mkuu ataandaa mpango mkakati, mpango wa biashara wa Mfuko na bajeti ya mfuko kwa kila mwaka wa fedha na kuiwasilisha kwenye Kamati ya Ushauri ili kuidhinishwa.

(2) Fedha zilizowekwa katika Mfuko zitatumika kama itakavyoidhinishwa na Katibu Mkuu baada ya kupokea ushauri wa Kamati ya Ushauri.

(3) Kwa madhumuni ya aya ndogo ya (2) hakuna fedha zitakazotumika isipokuwa kwa idhini ya Katibu Mkuu.

Salio la ziada

11. Mapato, malimbikizo na fedha nyingine mwishoni mwa mwaka wa fedha zitabaki katika Mfuko kwa madhumuni ya kuendelea kutekeleza majukumu ya Mfuko.

Mwaka wa fedha wa Mfuko

12. Mwaka wa fedha wa Mfuko utakuwa ni kipindi cha mwaka mmoja unaoanzia tarehe 1 Julai na kuishia tarehe 30 Juni ya mwaka unaofuata.

Hesabu, ukaguzi na taarifa ya mwaka

13.-(1) Katibu Mkuu ndani ya miezi mitatu ya mwisho wa kila mwaka wa fedha ataandaa taarifa za fedha kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za usimamizi wa fedha za umma.

(2) Taarifa za hesabu zitakazoandaliwa kwa mujibu wa aya ya (1) zitasainiwa na Katibu Mkuu na kuwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Dodoma,
7 Januari, 2023

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU,
*Waziri wa Fedha na Mipango*